

**SAALAM ZA MKUU WA MKOA WA PWANI MHE. ENG. EVARISTI W.  
NDIKILO KWA MHESHIMIWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO  
WA TANZANIA DKT. JOHN POMBE MAGUFULI KATIKA ZIARA YAKE  
KUHUSU UWEKEZAJI WA VIWANDA WILAYA YA MKURANGA  
MKOA WA PWANI TAREHE 6 OKTOBA, 2016**

- Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Dkt. John Pombe Magufuli,
- Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Pwani - Mheshimiwa Mwinshehe Mlao,
- Katibu Tawala wa Mkoa - Bw. Zuberi M. Samataba,
- Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga - Mhe. Filberto Sanga,
- Mbunge wa Mkuranga - Mhe. Abdallah Ulega,
- Viongozi wa CCM Mkoa na Wilaya ya Mkuranga,
- Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Mkuranga,
- Ndugu Said Salim Bakhresa - Mkurugenzi wa Kampuni ya Bakhresa Food Products Ltd.,
- Waandishi wa Habari,
- Wageni Waalikwa,
- Mabibi na Mabwana.

## **1. UTANGULIZI**

### ***Mheshimiwa Rais,***

Awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai uliotuwezesha kukutana hapa leo tukiwa salama. Pili, sisi Viongozi na Wananchi wa Mkoa wa Pwani kwa moyo wa dhati kabisa tunakukaribisha wewe na msafara wako hapa Mkuranga Mkoani Pwani katika ziara yako ya siku moja kutembelea kiwanda cha Chakula na Matunda cha Kampuni ya BAKHRESA FOOD PRODUCTS LTD. Tunasema karibuni sana.

### ***Mheshimiwa Rais,***

Hali ya Ulinzi na Usalama Mkoani Pwani ni shwari na wananchi wanaendelea na shughuli za uzalishaji mali. Yapo matukio madogomadogo ya kiuhalifu ya hapa na pale lakini vyombo vya dola vipo macho na vinaendelea kuyashughulikia kadri yanavyojitokeza.

### ***Mheshimiwa Rais,***

Kwa kuwa ziara yako ya leo imelenga kutembelea shughuli za uwekezaji hususani Ujenzi wa Viwanda, taarifa yetu itajikita zaidi katika uwekezaji wa viwanda na namna ambavyo Mkoa umejipanga kutekeleza maelekezo ya Serikali ya Awamu ya Tano kuhusiana na Viwanda.

## **2. HALI YA UWEKEZAJI WA VIWANDA MKOANI PWANI**

### ***Mheshimiwa Rais,***

Katika kuitikia kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya "Kujenga Uchumi wa Viwanda ili ifikapo mwaka 2025 Tanzania iwe nchi ya Uchumi wa Kati" Sisi tumeazimia kuufanya Mkoa wa Pwani kuwa Ukanda wa Uwekezaji wa Viwanda (Industrial Zone). Ili kutekeleza azma hiyo tumefanya yafuatayo:-

### **2.1 Kuainisha, Kutenga na Kupima ardhi kwa ajili ya Ujenzi wa Viwanda**

#### ***Mheshimiwa Rais,***

Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri zake tumeainisha kutenga na kupima maeneo kwa ajili ya kujenga viwanda kama ifuatavyo:-

- (i) **Halmashauri ya Kibaha Mji** - imetenga jumla ya hekta 1,450 katika maeneo ya Zegereni, Misugusugu na Mtakuja kwa ajili ya Viwanda vikubwa na vidogo. **Hekta 318** zimepimwa na **hekta 1,132** zimeandaliwa michoro ya Mipango Miji.
  
- (ii) **Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha** - Imetenga ardhi ya jumla ya **ekari 3,266** katika maeneo ya Disunyara **ekari 466** na Kikongo **ekari 2,800**. Eneo la Kikongo linamilikiwa na Kampuni ya Trans-continental ambalo lipo ndani ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mlandizi. Tayari limegawanywa kwenye Vitalu (Blocks) na

wawekezaji wa ndani na nje ya nchi wameanza kuomba viwanja hivyo kwa ajili ya uwekezaji wa Viwanda.

- (iii) **Halmashauri ya Kisarawe** - Imetenga ardhi yenye jumla ya **hekta 4,500** katika eneo la viwanda la Visegese ambapo **viwanja 291** vyenye ukubwa wa **ekari 6** vimepimwa na upimaji unaendelea. Aidha, kuna eneo lenye ukubwa wa **hekta 2,800** lililopo Kijiji cha Mihugwe Wilayani Kisarawe ambalo linamilikiwa na Kiluwa Group and Company Ltd ambalo kwa sasa lipo mbioni kupata hati miliki na baadaye michoro ya Mipango Miji. Mikakati ya Mmiliki ni kuanzisha "Kiluwa Village Processing Zone" ambayo itakuwa na uwekezaji wa aina mbalimbali ikiwamo viwanda. Tayari Makampuni makubwa 50 kutoka nchini China yameonyesha nia ya dhati ya kujenga viwanda Kisarawe.
- (iv) **Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo** - Imetenga jumla ya **hekta 12,500** (EPZA **hekta 9,800**, Mataya **hekta 1,200** na Matibwa hekta 1,500) kwa ajili ya Viwanda. Maeneo haya yanaendelea kufanyiwa uthamini na ulipaji wa fidia. Katika eneo la EPZA, kwa mfano, wananchi 2,180 walifanyiwa uthamini na kati ya hao wananchi 1,155 wamelipwa fidia.
- (v) **Halmashauri ya Wilaya ya Mafia** - Imetenga **Ekari 4,040** za ardhi katika eneo la Utumaini kwa ajili ya uwekezaji.
- (vi) **Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga** - Imetenga **ekari 7,450** za ardhi katika Vijiji vya Dundani **ekari 700**, Misufini, Kidete, Mponga na Ngarambe **ekari 4,000** na

Mkiu **ekari 1,000** kwa ajili ya Viwanda. Aidha, kuna eneo la ukubwa **ekari 1,750** katika Kijiji cha Magodani, Kazole na Lugwadu linalomilikiwa na Kampuni ya M/S Soap and Allied Industries Ltd. litakalotumika kwa ajili ya uwekezaji mbalimbali wa viwanda kwa wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi. Kwa sasa michoro ya Mipango Miji imepatikana na Wawekezaji wa ndani na nje ya nchi wameanza kuomba maeneo kwa ajili ya uwekezaji.

(vii) **Halmashauri ya Rufiji** na Kibiti - Imetenga **hekta 1,100** za ardhi katika eneo la Utunge Utete na limewekwa kwenye ramani ya Mji Mdogo wa Utete kwa ajili ya Viwanda. Aidha kuna Ardhi yenye ukubwa wa Ekari 25,000 ambazo zitawekezwa kwa ajili ya kiwanda kikubwa cha Sukari na kilimo cha Miwa.

### ***Mheshimiwa Rais,***

Tumeendelea kuzihimiza Halmashauri zetu kushirikiana na TANESCO, TANROADS na DAWASCO kuweka Miundombinu wezeshi kwa maana ya Umeme, Barabara na Maji kwenye maeneo yanayotengwa kwa ajili ya viwanda ili uwekezaji uende kwa haraka zaidi.

## **2.2 Kutangaza Fursa za Uwekezaji zilizopo Mkoani Pwani**

### ***Mheshimiwa Rais,***

Ili kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ya nchi, Mkoa umeandaa Wasifu wa Fursa za Uwekezaji (Coast Region Investment Profile) na kuzitangaza fursa hizo kupitia Tovuti ya Mkoa (Website), TIC

na Diaspora kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa na Ziara za mafunzo nchini China na Hongkong. Aidha, tunakusudia kufanya Kongamano la Uwekezaji kwa ushirikiano na wenzetu wa Mkoa wa Morogoro mwaka huu ambapo fursa za uwekezaji katika Mikoa hii miwili zitatangazwa zaidi.

### ***Mheshimiwa Rais,***

Sababu zinazotufanya Mkoa wa Pwani tuwe na fursa nyingi za uwekezaji wa viwanda ni hizi ifuatavyo:-

- (i) Uwepo wa ardhi ya kutosha kama nilivyoieleza hapo juu ambayo Halmashauri sasa zinatenga.
- (ii) Uwepo wa Miundombinu ya Barabara za lami, Reli za TAZARA, Kati na Reli ya Tanga, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNIA) na Bandari kubwa ya Dar es Salaam.
- (iii) Umeme na Maji ya uhakika kutoka Gridi ya Taifa na Vyanzo vya Maji vya Ruvu na Wami.
- (iv) Uwepo wa soko kubwa la Jiji la Dar es Salaam lenye watu karibu milioni nne (4).
- (v) Uwepo wa Ukanda mrefu wa Bahari ya Hindi unaofaa kwa ujenzi wa Hoteli za Kitalii na Viwanda vya Uchakataji Samaki.

## **2.3 Matokeo ya Juhudi za Mkoa**

### ***Mheshimiwa Rais,***

Juhudi zilizofanywa na zinazoendelea kufanywa na Mkoa zimeanza kuzaa matunda, kama ifuatavyo:-

- (a) Jumla ya Viwanda Vikubwa, vya Kati na Vidogo 88 vimejengwa na vinafanya kazi (Mkuranga viwanda 41, Kibaha Mji viwanda 10, Chalinze viwanda 24, Bagamoyo viwanda tisa (9), Kisarawe viwanda viwili (2) na Mafia viwanda viwili (2).
  
- (b) Miradi ya Kimkakati imeanza na ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi ama ipo njiani kuanza ujenzi; kama ifuatavyo:-
  - (i) Kiwanda cha Vigae (Tiles) cha Goodwill (Tanzania) Ceramic Co., Ltd kilichopo Mkuranga. Kiwanda hiki kinamilikiwa na Mwekezaji kutoka nchini China, na kinatarajiwa kuanza uzalishaji wa Vigae mwezi Desemba mwaka huu.
  
  - (ii) Kiwanda cha Nondo cha Mohamed Kiluwa Group and Company Ltd cha Mlandizi ambacho kinatarajiwa kuanza uzalishaji mwezi ujao.
  
  - (iii) Kiwanda cha Kusindika matunda, (Sayona Fruits) kilichopo Kijiji cha Mboga - Chalinze - Bagamoyo. Mwekezaji ni Makampuni ya MMI (Motisun Group) ambayo yatawekeza jumla ya Dola za Kimarekani

milioni 55. Kibali cha ujenzi (Building permit) kimepatikana na ujenzi uko mbioni kuanza.

- (iv) Kiwanda cha Saruji itakayojulikana kama "Mamba Cement" kilichopo Kijiji cha Talawanda na Magulumatali- Bagamoyo. Mwekezaji ni Makampuni ya MMI (Motisun Group). Nao pia kibali cha ujenzi kimepatikana na ujenzi uko mbioni kuanza.
- (v) Kiwanda cha Nondo cha MMI Intergrated Steel Mill kilichopo eneo la Zegereni, Halmashauri ya Mji Kibaha. Mwekezaji amepewa kibali cha ujenzi na ujenzi utanza wakati wowote.
- (vi) Eneo la Uwekezaji wa Viwanda, Maduka ya biashara, Makazi n.k lililopo Mlandizi - Kisabi "Block A na B" - Halmashauri ya Kibaha Vijijini, ambapo wawekezaji mbalimbali wamepewa viwanja na wanajipanga kuanza ujenzi ili kubadilisha kabisa mandhari ya Mji wa Mlandizi.
- (vii) Mradi wa Global Land Solution Ltd (Palacha Dream City) - Kisiju Mkuranga utakaohusisha ujenzi wa Hoteli, Nyumba za Makazi, Nyumba za biashara na Huduma za Kijamii kama Shule, Maji, Masoko, Hospitali na Nyumba za Ibada. Mradi huu unamilikiwa na Mtanzania Adamjee na tayari wamepata hati miliki. Kwa sasa wanawasiliana na Baraza la Taifa la Utunzaji wa Mazingira ili kufanya tathmini ya athari za kijamii na kimazingira ili hatimaye waendeleo na ujenzi.

## ***Mheshimiwa Rais,***

Uwepo na Viwanda vinavyofanya kazi na Miradi iliyoanza kujengwa itakapokamilika ni fursa muhimu sana kwa maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja, Mkoa na Taifa kwa jumla. Bila shaka Ajira na kipato kitaongezeka kwa wananchi na Serikali itapata mapato kutokana na kodi, ushuru na masoko kwa ajili ya bidhaa na huduma.

## **2.4 Changamoto**

### ***Mheshimiwa Rais,***

Pamoja na mafaniko tunayoyaona katika suala zima la uwekezaji, zipo changamoto kadhaa tunazokumbana nazo kama ifuatavyo:-

- (i) Migogoro ya ardhi kati ya Wananchi na Wawekezaji. Hii inatokana na baadhi ya wananchi kuvamia maeneo yaliyotengwa na kumilikiwa kihalali na wawekezaji. Aidha, baadhi ya wananchi kutoridhika na kiasi cha fidia kilichowekwa kwa mujibu wa sheria, hali inayosababisha pande husika kwenda mahakamani na kwa hivyo kuchelewesha uwekezaji. Ili kuondokana na changamoto hii tunawaelimisha wananchi kuhusu umuhimu na faida za uwekezaji. Aidha, Halmashauri zimeelekezwa kutenga na kuainisha maeneo hayo mapema kwa ajili ya uwekezaji.
- (ii) Gharama kubwa za uwekaji wa Miundombinu wezeshi kwa maana ya Umeme, Maji na Barabara. Ili kuondoa changamoto hii, tunahimiza ushirikiano wa Halmashauri na Mamlaka zinazohusika na ujenzi wa miundombinu husika

kama TANROADS, DAWASCO na TANESCO ili kuwa na mipango shirikishi.

#### **4. MWISHO**

***Mheshimiwa Rais,***

Kwa mara nyingine tena tunakushukuru sana kwa kutenga muda wako na kututembelea Wanapwani, pamoja na majukumu mazito ya kitaifa na kimataifa ulinayo. Tunakuomba kama itakupendeza, ufanye ziara nyingine itakayohusisha Mkoa wote wa Pwani ili uone shughuli za uwekezaji wa viwanda unavyoendelea. Aidha, ziara hiyo itakupa fursa ya kushuhudia juhudi zinazofanywa na wananchi wa Mkoa wa Pwani katika kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Rais, naomba kuwasilisha.

Eng. Evarist W. Ndikilo  
**MKUU WA MKOA  
PWANI**